

Mifugo na Uvuvi

Majukumu ya Idara ya Mifugo na Uvuvi

- Kubuni mipango ya uzalishaji mifugo.
- Kuratibu mipango ya ugani kuhusiana na mifugo.
- Kuratibu na kuendesha mafunzo ya ufugaji bora, usindikaji wa mazao ya mifugo kwa wataalu wa mifugo na wafugaji.
- Kubuni, kuanzisha na kutekeleza miradi ya maendeleo ya mifugo.
- Kutafiti maeneo mapya yanayofaa kwa ufugaji wa mifugo mbalimbali.
- Kufanya utafiti juu ya uihalibifu wa mazingira.
- Kushiriki katika shughuli za kudhibiti milipuko ya wanyama na viumbe waharibifu wa malisho.
- Kuandaa taarifa ya robo, nusu na mwaka juu ya maendeleo ya mifugo.
- Kufuatilia, kuweka, kuchambua na kutafsiri takwimu za uzalishaji wa mifugo.
- Kusimamia huduma zote za afya ya mifugo afya ya umma na wanyama.
- Kuandaa mipango ya muda mfupi na mrefu ya kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya wanyama.
- Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi, kusambaza na kutumia data za magonjwa ya mifugona taarifa nyingine.
- Kuratibu matumizi ya maji ya mifugo na uhifadhi wa maeneo ya malisho na vyanzo vya maji.
- Kuelimisha wafugaji juu ya matumizi bora ya nyanda za malisho.
- Kusimamia utekelezaji wa sheria za nyanda za malisho na vyanzo uzalishaji wa vyakula vya mifugo.
- Kuhamasisha utunzaji na uhifadhi wa nyanda za malisho kwa mbinu za asili.
- Kuelimisha na kuhamasisha matumizi ya mabaki ya mazao na masalia ya mazao.
- Kupunguza migogoro kati wafanya biashara wakubwa wa binadamu na wazalishaji wa vyakula vya mifugo.
- Kusajili na kusimamia sekta binafsi za mifugo.
- Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa nyama na ngozi.
- Kusimamia utekelezaji wa sheria ya mifugo na sheria ya ngozi.
- Kuhamasisha uzalishaji, ukusanyaji na utunzaji na uuzaji wa ngozi bora.
- Kuongeza thamani ya ngozi.
- Kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa ngozi.
- Kuhamasisha matumizi ya masoko bora ya mifugo.
- Kutekeleza sera ya uvuvi.
- Uhifadhi wa samaki na viumbe wengine wa majini na mazingira yao.
- Kuratibu na kusimamia uhifadhi wa mazingira.

- Kuendeleza uvunaji endelevu wa samaki na viumbe wengine wa baharini, maziwa, mito, mabwawa na malambo.
- Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uvuvi bora, utengenezaji na uhifadhi bora wa samakina mazao ya uvuvi, biashara na masoko ya samaki pamoja ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa majini.
- Kutoa leseni za uvuvi.
- Kuendesha mafunzo ya taaluma ya uvuvi.
- Kusimamia na kutekeleza sharia za uvuvi (k.m kuzuia uvuvi haramu).
- Kusimamia ukusanyaji wa takwimu za uvuvi pamoja na maduhuli.
- Kuratibu shughuli za utafiti wa uvuvi.
- Kutoa ushauri na mafunzo kwa wananchi juu ta uendelezaji na matumizi enelevu ya rasilimali za uvuvi.
- Kukagua ubora wa samaki na mazao ya uvuvi na kuweka viwango vya kitaifa.